

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



Anwani ya Simu: "ADMIN"
Simu Nambari: 028 – 2520025
028 – 252003552
Nukushi: 028 – 2520033
Barua pepe: ras.geita@tamisemi.go.tz
Tovuti: www.geita.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
Mkoa wa Geita,
52 Barabara ya Mkoani,
Sanduku la barua 315,
30180 GEITA

TAARIFA KWA UMMA
KUFANYIKA KWA MTHANI WA UPIMAJI WA TAIFA WA DARASA LA NNE
(SFNA) – 2023

Geita

Oktoba 24, 2023.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Geita inapenda kuutangazia umma kuwa, Mthani wa Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne (SFNA – 2023), utafanyika kuanzia tarehe **25-26/10/2023**, ambapo mkoa wa Geita ni miongoni mwa Mikoa **26** Tanzania Bara ambayo itahusika na mthani huu.

Aidha, Mkoa una jumla ya shule za Msingi **742** zenye watahiniwa wa SFNA 2023 ambapo kati ya shule hizo, **690** ni za serikali na **52** ni za binafsi. Hilo ni ongezeko la shule **43** sawa na asilimia **6** ikilinganishwa na shule **699** zilizofanya mthani kama huu kwa mwaka **2022**.

Kwa mwaka 2023, jumla ya watahiniwa **120,558** wamesajiliwa kufanya mthani huu kwa mkoa mzima, na kati yao wavulana ni **57,934** na wasichana **62,624**. Kati ya watahiniwa hawa, jumla ya watahiniwa **2,024** ni wa shule za binafsi.

Mchanganuo wa Watahiniwa kwa kila halmashauri ni kama ifuatavyo:

		JUMLA KUU		
		WAV	WAS	JML
1	GEITA TC	5,436	5,683	11,119
2	GEITA DC	22,531	24,755	47,286
3	BUKOMBE DC	7,285	8,014	15,299
4	CHATO DC	12,657	13,002	25,659
5	MBOGWE DC	6,731	7,266	13,997
6	NYANG'HWALE DC	3,294	3,904	7,198
		57,934	62,624	120,558

Hivyo basi, kupitia taarifa hii, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inatoa wito kwa wazazi na walezi kuwapa ushirikiano watahiniwa hawa ili waweze kushiriki vyema kufanya mthani wao na tunawatakia mafanikio mema.

Boazi Mazigo,
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
RS-GEITA.